TANZANIA HIGHER LEARNING INSTITUTIONS TRADE UNION
P.O. BOX 11727, DAR ES SALAAM
Email: katibu@thtu.biz.tc, mtalo@thtu.biz.tc
Mobile: +255 755 576 224
Website: http://thtu.biz.tc

Kumb. Na. THTU/C/2009/122 Tarehe: 25/06/2009

Msajili wa Hazina,
Wizara ya Fedha,
S.L.P 9111,
Dar es salaam.

**YAH: UTEKELEZAJI WA SHERIA YA BIMA YA AFYA**

Rejea kichwa cha barua hapo juu.

Chama chetu kimepokea malalamiko kutoka kwa wanachama wetu waliopo katika Taasisi za Elimu ya Juu kwamba ofisi yako imetoa maelekezo yanayoonyesha kwamba Taasisi za Elimu ya Juu, zinapaswa kujiunga na Huduma ya Mfuko wa Afya (NHIF).

Chama chetu kimepitia sheria tajwa na sheria nyingine za nchi, ikiwemo sera na sheria ya utumishi wa umma, sheria za mifuko ya hifadhi ya jamii, katiba ya nchi, sheria za kazi na mikataba ya kimataifa inayohusu kazi na haki za mfanyakazi, ambayo Tanzania imeridhia, na kugundua kwamba kuna dosari za msingi katika sheria na utaratibu uliotumika, hivyo kufanya utekelezaji wake ukose uhalali kwenye Taasisi za Elimu ya Juu.

Kwakuwa suala hili ni nyeti na utekelezaji wake unaweza kuibua mgogoro mkubwa katika taasisi zetu dhidi ya Serikali, tunashauri kuwa na mazungumzo na ofisi yako ili kulipatia ufumbuzi suala hili. Pia tunaomba busara itumike kuondoa uharaka wa utekezaji wa suala hili mpaka pale majadiliano baina ya chama na ofisi yako yatakapokamilika.

Chama chetu kinashauri maelekezo yaliyotolewa kwa viongozi wa taasisi husika utekelezaji wake usubiri matokeo ya fursa ya majadiliano kati ya chama na ofisi yako.

Ni matumaini yetu kwamba ofisi yako itaandaa utaratibu wa haraka kukutana na viongozi wa chama chetu mapema iwezekanavyo.



Dk. E.G. Mtalo,
Mwenyekiti THTU Taifa

**Nakala:** Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
Ikulu – Dsm.

Mhe. Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
Ikulu -Dsm.

Mhe. Waziri wa Fedha
Dsm.

Mhe. Waziri,
Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma
Dsm.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi
Dsm.

Mhe. Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana
Dsm.

Mwenyekiti
CVCPUT
Dsm.

Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Umma,
Tanzania.

Wakuu wa Vyuo Vikuu Vishiriki,
Tanzania.

Wakuu wa Taasisi na Vyuo vya Elimu ya Juu,
Tanzania.

Wenyeviti wa Matawi ya THTU
Tanzania.